

UFUNGUO WA MLANGO

 Majaliwa kuwa kwenye maskani! Kidogo lilikuwa ni jambo lisilotarajiwa kwangu, pia. Mimi, nikijua usiku wa leo ulikuwa ni usiku wa ushirika, daima mimi napenda, kama nikiwa mahali popote karibu na hapa, nije kwenye ushirika. Kwa sababu ni... Nafikiri kwamba Wakristo wote wanapaswa kushiriki katika kula ushirika, kwa kuwa Yesu alisema, “Msipoula, hamna shirika Nami.” Kwa hiyo, ni ninii... daima ni majaliwa makuu ku—kuja maskanini. Halafu, usiku wa leo, Ndugu Neville alisema alikuwa kidogo amepwelewa na sauti, na—na alipenda kama ningezungumza na kusanyiko letu. Nikamwambia ningefurahi kufanya hivyo. Ningetaka kutangaza pia kwamba kama...

² Kesho usiku ni mkutano wa wanaume, wadhamini, kesho usiku, na wafanya biashara hapa wa kanisani, kwenye mkutano wao wa kawaida wa Jumatatu usiku na ninii yao... wana maamuzi ya kufanya pamoja na mkandarasi. Nadhani nyote mnaelewa ya kwamba ninii zetu—ninii zetu—hati zetu zilifaulu, nasi tutaweza kulijenga kanisa. Na kwa hiyo zimefaulu, na labda tutaanza juma hili. Kanisa linaanza juma hili, kadiri ni juavyo mimi. Nao walitukatalia, hapa Jeffersonville. Lakini tulienda Indianapolis, jimboni, nao wakaturuhusu, kwa hiyo tatalijenga. Na kwa hiyo linaanza, labda, juma hili. Itajulikana baada ya mkutano wa kesho usiku. Na kisha baada ya mkutano kesho usiku, kama hawaanzi juma hili, kama jambo fulani likitukia, mkandarasi hawezi kuanza juma hili, basi ataanza juma lijalo.

³ Na wikiendi hii ijayo, Jumamosi usiku, Jumapili asubuhi, na Jumapili usiku, ya juma lijalo, Jumamosi hii ijayo na Jumapili, Bwana akipenda, ninataka kufanya m—m—mkutano wenye vipengele vitatu kwa pamoja, tena, kama tulivyofanya majuma machache yaliyopita. Na ndipo baada ya sisi... Hiyo itakuwa ni Jumamosi usiku, na kisha Jumapili asubuhi, na halafu Jumapili usiku. Huu ujao, hiyo itakuwa ni tarehe kumi na tatu na kumi na nne za mwezi huu.

⁴ Na halafu baadhi ya ndugu pamoja na mimi tutaondoka baada ya wakati huo, kwenda huko Colorado, katika ziara ya kuwinda, kisha turudi. Kama maskani, wakati itakapomalizika, ikiwa ni mapenzi ya Bwana, ninataka kuchukua, labda, juma zima kabla sijaondoka tena kwenye mikutano, na kuchukua *Ile Mihuri Saba* ya Ufunuo. Kabla tu... Kama vile tulivyokuwa na zile *Nyakati Saba Za Kanisa*, sasa ile *Mihuri Saba* itazifuata Hizo.

⁵ Na labda katika kama majuma mawili ama matatu yafuatayo, kwa sababu nafikiri wanadai wao, pamoja na mtu

watakayempa mamlaka juu yake, wanaweza, tunaweza kuijenga maskani na iwe tayari katika muda wa siku kumi hivi, ama kumi na tano, kitu kama hicho. Ndipo tutakuwa na nafasi hapa ya kuketi kadiri ya mara mbili ya watu tulio nao, ama mara tatu, labda watu zaidi. Na hivyo ndivyo nilivyokuwa nikingojea kufikia wakati huo.

⁶ Kwa sababu, ile Jumamosi na Jumapili zilizopita, hali ilikuwa mbaya sana, mnajua. Watu walikuwa wamesimama hapa nje kwenye saa nane alasiri, kuijaza maskani, kabla kanisa halijafunguliwa bado. Kesho yake asubuhi, kwenye saa kumi na moja, nesi aliye jirani yangu, akija kutoka huko juu, alisema, “Watu walikuwa wamesongamana kuizunguka maskani yote saa kumi na moja alfajiri.” Kwa hiyo, na ndipo hao watu, wanapoingia, hakuna nafasi, nao wanavunjika moyo na kuondoka. Na—na halafu hao wanaosimama, na kulundikana na wamesongamana kwenye marefu ya kanisa, wanajisikia wamebanana sana, na kila kitu. Nami ninawaona wanawake wamesimama pale, wakitokwa na jasho, mwajua, namna hiyo, na jasho likiwatiririka. Na mwanamume fulani anasimama na kumpa ninii chake, mwanamke fulani kiti; ndipo atasimama mpaka miguu yake inauma, na mtu mwingine atampa. Mwajua, na jinsi hiyo, na ni la kuhuzunisha, na akina mama na watoto wao wachanga wagonjwa na kadhalika, hilo ni jambo baya.

⁷ Kwa hiyo, tunajaribu kuondoa hilo kwa kujenga maskani kubwa zaidi. Na tutakuwa na mahali pazuri ambapo watoto, wakati mwingine...na kukatiza, kama vile watoto wadogo wakilia; vema, tutakuwa na chumba kwa ajili ya jambo hilo, ili akina mama waweze kuingia, wangi wakiiona ibada, na itangazwe moja kwa moja humo chumbani. Na kuwa na vyumba vya shule ya Jumapili na kila kitu vikiwa vimewekwa tu jinsi vinavyopaswa kuwa. Na hilo, Bwana akipenda, linatendeka, litatendeka juma hili lijalo.

⁸ Nyote mlilipigia kura asilimia mia moja, kwa hiyo tumelishikilia jambo hilo moja kwa moja, mnaona. Kanisa linajitawala lenyewe. Yale kanisa lisemayo, hayo ndiyo. Wadhamini wala isiwe mtu mwingine yeyote...Wadhamini ni ninii tu, kila mmoja, ni kura moja. Mchungaji ni kura moja tu. Kanisa ndilo, hiyo ni—ni demokrasia ya kanisa, kujitawala kwa kanisa. Kanisa, kwa ujumla, hunena. Hivyo tu. Nasi tunapenda jambo hilo, kwa kuwa hatuna maaskofu wala utawala msonge wala waangalizi ama kadhalika kutwambia *hivi, vile*, ama *vinginevyo*. Ni Roho Mtakatifu kanisani, anayenena. Ninapenda utawala huo, na ni mzuri sana.

⁹ Nami niliuliza, “Je! nyote mlitaka kungojea mpaka tutakapopata za kutosha kuihamisha maskani na kujenga kanisa kubwa?” Hilo lilikuwa kwenye halmashauri ya wadhamini, wala lisingeweza kutatuliwa na wadhamini. Na ndipo wakaniomba, kama kiongozi mkuu, nije nikaliulize

kanisa. Kwa hiyo nikasema, “Sasa tuna fedha za kutosha kuongezea ukubwa wa kanisa na kulitengeneza vinginevyo kabisa, na kadhalika, kuliko kile tulichokuwa nacho.” Nikasema, “Sasa tunaweza kufanya hivyo mara moja, ama tuweke akiba fedha zetu mpaka tutakapopata za kutosha kujenga kanisa zima, jipya, mahali pengine.”

¹⁰ Na tulilipigia kura kanisani, na kwa kauli moja ikapigiwa kura ya “kujenga kanisa sasa hivi, na ni kujenga tu kanisa kubwa zaidi sasa hivi.” Nasi tumeshikilia hilo.

¹¹ Na halmashauri hapa Jeffersonville ikatukatalia, ikasema tusingeweza kufanya hivyo. Nasi tukaivuka hiyo, tukaenda Indianapolis na kuuhusisha Mkoa katika hilo. Na ndipo wakatuma jibu, kwamba, “endeeleni,” tuna ruhusa ya kulijenga. Kwa hiyo basi jiji hili halina uhusiano nalo sasa, Mkoa ndio unaopaswa kulishughulikia. Hivyo basi tunayo ruhusa, na mkandarasi anayo i—idhini mkononi mwake sasa hivi, na ninadhani wako tayari kuanza wakati wowote.

¹² Kesho hii usiku, kama nanii—kama mkandarasi akisema anataka kuanza juma lijalo, basi nitafutilia mbali tu mikutano ya ninii...mpaka tutakapofikia kwenye *Ile Mihuri Saba*. Na halafu kama mkandarasi hawezi kuanza juma lijalo, basi Jumapili inayofuata, Jumamosi na Jumapili, nitafanya mkutano kabla ya kuondoka.

¹³ Na basi nilikuwa niufanye Jumapili hii, ndipo nikakuta kwamba usiku wa leo ni usiku wa ushirika, kwa hiyo nikauacha Jumapili hii. Kwa sababu, umati kama huo, huwezi kufanya ushirika kwa utulivu, na kisha tutakapokuwa na kanisa kubwa zaidi tunaweza.

¹⁴ Sasa, tuna Rais anayekuja. Nanii...loo, mnajua ninalomaanisha, ndio kwanza atolewe kwa familia ya Hickerson si muda mrefu uliopita. Naye dada yetu ambaye ni mpiga piano, kama atakuja atupe sauti ndogo kwenye piano, ya “Walete,” tafadhali, ama wimbo fulani mfupi wa jinsi hiyo. Huyu mwungwana mdogo na mzuri katika familia ya Hickerson, ambaye ametazamiwa kwa muda mrefu sana, amewasili. Jamaa mdogo mzuri sana, na hakika yeye ni johari kwa jamii ya Hickerson. Nao wote ni johari kwetu, tunawapenda na kweli wao ni ndugu na dada yetu. Tunashukuru kuwa na huyu mtoto kuzaliwa katika familia yao, jambo ambalo limeibadilisha kabisa familia hii. Nawaomba, baba na mama wamlete mtoto huyu mchanga sasa kwa ajili ya kuwekwa wakfu. Sasa, Maandiko yanasema, “Wakamletea watoto, wachanga, ili aweke mikono Yake juu yao na kuwabariki.”

¹⁵ Sasa, wapo watu ulimwenguni wanaoamini katika kile wanachokiita “ubatizo wa watoto wachanga.” Na, hiyo ni kusema, wanawachukua watoto hawa wadogo na hawawabatizi hata kidogo, maana, wao wanawanyunyizia tu maji. Sasa,

hatuoni jambo hilo popote katika Biblia, ambapo walipata kamwe kumnyunyizia mtu yeyote, watu wazima, licha ya watoto.

¹⁶ Na kwa hiyo ubatizo ni kukiri kwamba kazi ya ndani ya neema imekwisha kufanyika. Na watoto hao wachanga hawana habari na dhambi. Kwa hiyo, wakati Yesu alipokufa msalabani, Yeye alikufa apate kuiondoa dhambi ya ulimwengu. Basi wakati mtoto mchanga anapokuwa mwanadamu, na anazaliwa humu ulimwenguni, wao hawana dhambi yao wenyewe, kwa hiyo hawana toba la kufanya. Bali, wakati hiyo, Damu ya Yesu Kristo huiondoa hiyo dhambi. Hakika, mtoto huyo mchanga amezaliwa katika dhambi, ameumbika katika uovu, anakuja ulimwenguni akisema uongo, nao asili yao ni wenye dhambi, bali Damu ya Yesu Kristo huwapatanisha kwa hiyo. Lakini wakati mtoto huyo mchanga anapofikia umri wa kuwajibika, naye anajua mema na mabaya, basi hana budi kutubia yale amefanya. Dhambi yake sasa ni dhambi kama tu jinsi alivyozaliwa katika dhambi, ni dhambi ya kibinadamu, dhambi hiyo sasa ni dhambi ambayo Adamu na Hawa waliifanya; na ambayo iliondolewa na Mungu, kwa Damu ya Yesu Kristo. Sasa mtoto huyo mchanga hana dhambi ya kutubia mpaka atakapotenda dhambi, ndipo hana budi kutubu. Unaona? Na wakati anapotubu, basi huo ndio wakati wa kubatizwa, na kisha anabatizwa kwa kuzamishwa.

¹⁷ Hadi wakati huo, sisi tunafuata mafundisho ya Biblia, ambayo, “Walimletea Yesu watoto wadogo, ili aweke mikono yake juu yao na kuwabariki.” Mzazi huyu mpendwa usiku wa leo anamleta mtoto huyu mchanga kwangu mimi na mchungaji, awekwe wakfu. Nao wanajisikia ya kwamba kumweka mikononi mwa wawakilishi wa Kristo, wao wanamweka mikononi mwa Kristo. Kwa hiyo, kwa imani, sisi tunampeleka mtoto huyu mchanga kwa Mungu, kutoa shukrani kwa kumleta hapa, na kumwomba Mungu ambariki, jambo ambalo tunaliita “kuwekwa wakfu kwa mtoto mchanga.”

¹⁸ Sasa, mnajua jinsi ambavyo ngingekuwa kwa watoto wangu mwenyewe. Nina msichana mdogo Utukufuni usiku wa leo, naye aliwekwa wakfu kwa Bwana, hapa madhabahuni. Nina mvulana mdogo na msichana wanaoketi pale nyuma, usiku wa leo, ambao hawajabatizwa bado. Mmoja, miaka kumi na moja, nimekuwa nikizungumza naye kuhusu jambo hilo leo hii, Sara, kwa ajili ya ubatizo. Na Joseph ana saba tu, kwa hiyo yeye bado ni mdogo sana kwa huo, kadiri mpaka... Kama angeutaka, na aseme Mungu alikuwa akiuweka moyoni mwake, ningembatiza basi. Lakini, kama watoto wachanga, mimi huwaweka wakfu tu kwa Bwana, maana hilo ndilo fundisho la Kimaandiko la jambo hilo.

¹⁹ Ndugu Neville, naomba utoke pamoja nami sasa tuelekee kwa mvulana huyu mzuri. [Ndugu Branham anawakaribia Ndugu na Dada Hickerson—Mh.] Nilihofu... Je! Huyo ni Hollin? Hollin? Naam, Hollin, Junior. Stephen Hollin. Vema, hilo ni

sawa. Loo, nilidhani alikuwa amelala. Hiyo ni ile tabia ya jamii ya Hickerson, lolote linaloendelea. Nilimwona hivi majuzi, nikasema “Rais,” na kadhalika. Na, hakika, hilo lilikuwa ni jambo dogo sana kwake, mnaona, kumwita “Rais.” U hali gani? Vema, ninajua hiyo inabidi kuwa ni hazina kwa mama yeyote mcha Mungu. Waonaje wewe? Mzuri sana. Na sasa, Ndugu Hickerson na Dada Hickerson, kama mtumishi wa Kristo, kama mchungaji wenu, ninamchukua mtoto huyu mchanga, kwa imani, kumweka kwenye mikono ya Yesu Kristo, ambaye mnataka kumweka mikononi Mwake.

²⁰ Na tuviinamishe vichwa vyetu wakati mimi na mchungaji tukisimama hapa huku mikono yetu ikiwa juu ya mtoto huyu mchanga.

²¹ Baba yetu wa Mbinguni, katika Biblia walikuletea watoto wachanga, upate kuweka mikono Yako juu yao na kuwabariki. Na kwa kweli, Bwana, walibarikiwa. Na sasa kuufuata mfano Wako, mambo uliyoyafanya, tumejaribu kwa makini, Bwana, kuisoma Biblia na kuufuata mfano huo kama tu ulivyofanya Wewe. Na baba huyu na mama, Ndugu na Dada Hickerson, wanafunzi wetu wapendwa hapa Maskanini, wanatuletea sehemu hii ndogo ya shangwe ambayo umeiweka katika malezi yao. Alitoka Kwako, Bwana. Uliwapa mtoto huyu. Na sasa wao wanataka kukupa Wewe maisha yake ya utoto, kuwa utumishi Kwako. Ninaomba ya kwamba umbariki mtoto huyu, ya kwamba Wewe utampa maisha marefu. Jalia aishi, ikiwezekana, apate kuona kule Kuja kwa Bwana. Ninaomba ya kwamba utambariki popote alipo. Jalia alelewe katika nyumba ya Kikristo, kama vile amezaliwa katika moja. Na jalia aendeele kwenye nyumba hii. Jalia baba na mama waishi wapate kumwona mtoto huyu mchanga mimbarani, ikiwezekana, akihubiri Injili. Wao ingekuwa heri wamwone jinsi hiyo, Baba, kuliko kwenye ki—kiti cha enzi katika Ikulu, ama mahali pengine popote, kwa kuwa wao ni watumishi Wako, nao wangependa maisha ya mtoto huyu mchanga yawe ni wakfu na baraka kwa kazi ya Mungu.

²² Sasa ninaomba, Baba, ya kwamba umbariki mtoto huyu. Na jalia neema ya Mungu ije juu yake, na jalia awe na afya na furaha maishani mwake mwote. Na jalia baba na mama waishi wapate kumwona akiwa mtu mzima, tunaomba tena. Mbariki tunayambariki katika Jina Lako.

²³ Na sasa, mtoto Stephen Hollin Hickerson, ninakutoa kwa Yesu Kristo, kusudi baraka tulizoomba zije juu yako. Uwe mwenye afya na mwenye nguvu, ndugu yangu mdogo, na uishi upate kumtukiza Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba hayo. Amina.

Mungu akubariki. Mungu awabariki ninyi nyote. Mtoto mzuri sana.

Ambako hatutazeeka kamwe, kamwe
 hatutazeeka,
 Kwenye nchi ambako hatutazeeka kamwe;
 Kamwe hatutazeeka, kamwe hatutazeeka,
 Kwenye nchi ambako hatutazeeka kamwe.

24 Hivi haitakuwa ni nzuri sana? Watoto watakuwa watu wazima, na wazee watakuwa vijana. Sasa, hilo si ni la ajabu? Wala kamwe hatutakuwa wagonjwa, wala hatutapata huzuni, wala hatutakufa kamwe.

25 Sasa, ibada, Ndugu Neville ametangaza. Ninataka kutangaza sasa, pia, ya kwamba mkutano huo, msiusahau, na mikutano ambayo ameitaja. Pia, Bibi Ford ambaye alikuwa amezoea kuja kanisani miaka mingi iliyopita, ndiyo kwanza nimpeleke kwa binti yake, siku kadhaa zilizopita, naye ana umri wa miaka themanini, naye alienda kukutana na Bwana jana usiku saa mbili, nadhani. Na ibada zake, mimi pamoja na mchungaji tutazifanyia kwenye lile kanisa dogo huko Coots, Jumatano, saa nne—nne na nusu, Jumatano hii ijayo. Bibi Ford, Bibi... Nafikiri nasahau ninii lake... Levi, Bibi Levi Ford. Nanii wetu... Huyo ni—huyo ni mama wa Lloyd Ford mnayemwona kwenye kitabu changu, kwamba alikuwa yuaenda kunihifadhia ile suti ya Skauti, nami nilipata tu soksi moja ndefu iliyosalia. Sasa, huyo—huyo ndiye mama wa mvulana huyo. Kwa hiyo nilimchukua hivi majuzi na kuomba pamoja naye, maskini kizee hicho. Naye akaenda kukutana na Bwana Yesu.

26 Sasa, Bwana akipenda, nilikuwa na kitu fulani hapa ambacho huenda nikatangaza ya kwamba zile ibada, kama zikiweko kwa juma hili lijalo, kama nimeziweka hapa ndani, ama angalau nilidhani niliziweka, kuhusu yale niliyokuwa ninaenda kuzungumzia kwenye—kwenye—kwenye ile ijayo, ibada hii ijayo ya juma lijalo. Kama na—nawazia... Nilidhani nililiweka katika kitabu hiki, sijui kama nililiweka ama la. Naam, hili hapa. Bwana akipenda, Jumamosi usiku ninataka kuhubiri juu ya somo la “Ni kwa nini mtu mmoja huyashawishi maisha ya mtu mwingine.” Kisha Jumapili asubuhi ninataka kuhubiri juu ya “Kufunikwa kwa Piramidi.” Na jumapili usiku ninataka kuhubiri juu ya *Kiongozi Wangu*, somo, *Kiongozi Wangu*, kwa ajili ya Jumapili hii ijayo usiku. Sasa Bwana na ayabariki mambo hayo na anisaidie, kwa kuwa nimekuwa nje, na somo fupi tu ili kuyaleta.

27 Sasa usiku wa leo, tunataka kuharakisha na kupata mambo machache. Jambo lingine, ninayo barua hapa ambayo—ambayo ndiyo kwanza itoke posta, kama Billy alivyoichukua muda mfupi uliopita, kwamba ndugu wengine wako Michigan, na hii imetoka kwenye shirika la wahudumu ambalo lina mambo mengi sana. Hilo ndilo linaloyatatiza mambo, mnaona. Hilo, wao wanadai humu ndani ya kwamba ndugu wengine huko juu ambao walisema ya kwamba niliwatuma huko juu, nao

wanahubiri ya kwamba wanamume wanapaswa kuwaacha wake zao na kumtafuta mwenzi wa kiroho, na kwamba—kwamba mimi kamwe siwezi kukosea kabisa. Ya kwamba hakuna kitu...Na, loo, baadhi ya mambo mabaya sana mliyopata kusikia. Nalo shirika la wahudumu likapata fununu yake, nao wananiandikia barua kuhusu jambo hilo, na ya kwamba niliwatuma huko juu na inasababisha vurugu kubwa sana. Na wengine wao wakitabiri na kusema ya kwamba mwanamume mmoja anapaswa kumwacha mke *huyu* na aende akamwote *yule*. Sasa, kanisa hili linajua ya kwamba hatuutetei upuuzi kama huo.

²⁸ Tunaamini katika Biblia. Tunaamini ya kwamba mwanamume anapomchukua mwanamke, huyo ni mkewe, na mauti pekee ndiyo inayoweza kuwatenganisha. Ni hayo tu. Hatuamini upuuzi kama huo. Wala hatuamini katika mapenzi ya kiholela. Hatuamini katika upuuzi huo. Tunaamini Biblia kabisa, na Hiyo peke yake. Kwa hiyo nitainakili tu, nakala ya barua hii, na kutoa jibu langu kwake na kuliweka kwenye magazeti, na hilo—hilo litashughulikia jambo hilo. Natumaini litalishughulikia, kwa vyovyote, kuwajibu.

²⁹ Sasa usiku wa leo, kabla tu hatujayafungua Maandiko, hebu na tuseme na Bwana wetu.

³⁰ Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia Kiti Chako cha rehema, katika Jina la Bwana Yesu, Yule mkuu aliyeshuka kutoka Utukufuni apate kutufunulia utajiri wa hazina za Mungu. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya Yesu huyu mkuu ambaye alikuwa ndiye dhihirisho la Mungu, lililofanyika kwetu binafsi, na kwa kupitia Yeye tuna ukombozi kutoka dhambini mwetu. Na sasa tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa kuwa tunamwamini Yeye. Kwa kuwa imeandikwa juu Yake, ya kwamba Yeye alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele; wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.”

³¹ Yabariki Maneno Yako, usiku wa leo, Bwana. Nasi tupo hapa kula ushirika katika muda mfupi tu. Mkristo, wenyeji wenzetu wa ule Ufalme watakusanyika kuzizunguka madhabahu, na hapo watakula tunachoita “ushirika,” ile se—sehemu ndogo ya—ya sakramenti ambayo Wewe umetuachia, kuonyesha ya kwamba tunaamini kwamba umekufa kwa ajili ya dhambi zetu, na kufufuka tena katika siku ya tatu, na u hai milele, na tunafanya jambo hili mpaka utakaporudi, kulingana na Maandiko kama vile tulivyoamriwa. Itakase mioyo yetu na mawazo mabaya na yote yale tumefanya ambayo yalikuwa ni kinyume na mapenzi Yako makuu. Baba, tusamehe, na utupe neema Yako usiku wa leo. Tumegee sasa Mkate wa Uzima, katika Neno, tunapolisoma na kuzungumza juu Yake. Katika Jina la Bwana Yesu, tunaomba hayo. Amina.

³² Sasa katika Kitabu cha Ufunuo, kuanzia na kifungu kimoja tu, ningetaka kusoma kifungu cha 20, ama kifungu cha 1 cha mlango wa 20.

Kisha nikamwona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake.

³³ Sasa ningependa kuzungumza, kama ingekuwa, kama ningeliita somo kutoka kwenye hili, ama kutoa somo kwenye kifungu hiki, kwa dakika zingine ishirini ama ishirini na tano, ningetaka kuliita, *Ufunguo Wa Mlango*. Sasa, sitaki ku—kulifanya “funguo,” kwa sababu Petro alipewa “funguo za ule Ufalme.” Ila ninataka kuliita hili: *Ufunguo Wa Mlango*. Na halafu mara baada ya jambo hili, ninataka kutoa matamshi machache madogo juu ya ushirika, kabla hatujaula usiku wa leo.

³⁴ Sasa, ufunguo. Ninaona hapa tunaposoma, ya kwamba Malaika huyu alishuka kutoka Mbinguni, akiwa na ufunguo mkononi mwake. Ninaamini ni Ufunuo 13 ama 19, tunaona tena, Malaika mwingine akija na ufunguo. Nao ufunguo ni, kusudi la ufunguo, ni kufungua kitu fulani, kitu ambacho kilikuwa kimefungwa, ama kitu ambacho kinapaswa kufungwa. Bali ufunguo unatolewa kwa kusudi hilo.

³⁵ Sasa, kuna aina nyingi za funguo, kwa sababu tuna matumizi mengi ya funguo. Kuna funguo za maghala. Kuna ufunguo wa nyumba yako mwenyewe, kuna ufunguo wa gari lako. Nasi tunaziita funguo, nazo ni funguo. Nazo zinaweza kurudufiwa, mara nyingi. Ama kwa nyumba, wakati mwingine waweza kufanywa, ule tunaouita, ufunguo malaya. Kwa maneno mengine, ni ufunguo ambao kwa namna fulani umefanywa kwa nyenzo, unatumika kwake, ambao—ambao unalizingusha kufuli kwa namna fulani na unaweza kufungua karibu mlango wowote, unaitwa “ufunguo malaya.” Ni kiunzi cha funguo nyingi, na unaweza kufunguliwa jinsi hiyo, kwa nyumba zetu ama hata kwa magari yetu, unaweza kurudufiwa. Halafu kuna . . .

³⁶ Ufunguo wowote hauwezi kuufungua mlango wowote mpaka umetumiwa na mkono. Kunapaswa kuwe na kitu cha kuutumia ufunguo. Ufunguo wenyewe hauwezi kujitumia. Inabidi kuwa na kitu fulani cha kuutumia huo ufunguo.

³⁷ Ni kama maikrofoni hii ambayo mimi—ambayo ninazungumza kupitia. Maikrofoni hiyo ni bubu. Isipokuwa pawe na kitu cha kuzungumza kuipitia, haiwezi kujizungumzia. Inabidi pawe na kitu fulani cha kuzungumza kuipitia. Kwa hiyo, sio maikrofoni, ni ile sauti ama ke—kelele (nyuma yake) ambayo maikrofoni inapitisha kwenye ma—mawimbi ya hewa, mpaka sikioni mwako.

³⁸ Sasa, hivyo ndivyo ilivyo katika kuihubiri Injili. Sio sisi wenyewe, kama wahudumu, sisi sio Injili. Bali sisi ni wapelekaji

tu ambao wanaipeleka Sauti ya Mungu kupitia kwenye uwakala wetu, wa binadamu, kumpelekea msikilizaji.

³⁹ Ono ni vile vile. Sijui kitu cha kuliambia kanisa wakati huu kuhusu ono. Lakini kama Roho Mtakatifu angenionyesha, kwanza, ono, ndipo ningelipeleka ono hilo kwa yule liliyelekezewa. Kwa hiyo halikuwa ni langu, mimi, hilo ono halikuwa ni langu, mimi. Mungu ndiye aliyetoa hilo ono, nami nikatumika kama mpelekaji, kuuleta ujumbe wa ono hilo kwa watu.

⁴⁰ Sasa, ufunguo ni kitu kile kile. Samahani. Ufunguo unapaswa tu kushikwa na mkono ambao unaufungua mlango. Mnaona, hauna budi uwe ni mkono. Sasa, na katika ufunguo nitakaozungumzia usiku wa leo, kuna mkono mmoja tu unaoweza kuushika ufunguo huu, na huo ni mkono wa Imani. Ndicho kitu pekee kinachoweza—kinachoweza kuushika ufunguo huu. Nayo mikono huzishika funguo zingine, na inahitaji mkono wa Imani kufanya jambo hilo.

⁴¹ Sasa, hebu na tuchukue kwa mfano ufunguo wa maarifa. Sasa, mtu hana budi kuninii, kama anajaribu kujiongezea maarifa, unaona, sasa, kuna ufunguo wa jambo hilo. Kuna njia ambayo mtu huyu hana budi kufungulia. Hana budi kufanya hivyo, kuchukua vitabu vyake na kisomo chake, wala hawezi...hakuna mtu anayeweza kumwelimisha. Huenda wakamfundisha, bali hana budi kuelimika. Na jinsi pekee inavyoweza kutendeka, yeye hana budi kuushika ufunguo huo, kitu fulani mle ndani kinachofungua ama ku... kinachomfunulia maarifa anayoyatafuta.

⁴² Na kuna watu kwa mfano ambao wangejaribu kucheza piano, nao...ama muziki. Hawajui kabisa jinsi ya kufanya jambo hilo, bali wangeweza kwenda pale na huenda mwalimu akachukua somo baada ya somo, wala kamwe wasingeufahamu. Kamwe hawawezi kuushika ufunguo wa siri hiyo, jinsi ambavyo mfuatano wiano na kubadilika kwa sauti na kadhalika unavyosikika. Inahitaji ufunguo.

⁴³ Na hisabati, kuna ufunguo wa hisabati, ambao unapaswa tu kupata uzoefu wake. Nimewaona watu ambao wangechukua safu nne za tarakimu, na kuziwekea vidole vyao, kila kimoja cha vidole vyao kwenye safu moja ya tarakimu, nao wanavishusha moja kwa moja namna *hiyo* kwenye kina cha tarakimu nne, na wanaweka jawabu hapo chini. Wakihesabu safu nne kwa wakati mmoja, popote pale kutoka moja mpaka tisa. Vema, nina wakati mgumu kuhesabu safu moja, isipokuwa niwe na vidole vya kutosha vya mikono na miguu kuhesabu, ku—kuhesabu safu moja. Kamwe nisingeweza kupata ufunguo huo. Lakini, unaona, baadhi yao hasa wana huo ufunguo wake, wanajua jinsi ya kutekeleza jambo hilo.

⁴⁴ Pia kuna ufunguo wa maarifa, mtu anayetafuta maarifa. Kuna ufunguo wa sayansi, utafiti wa kisayansi. Sasa, kuna, huo ni ufunguo mkuu. Watu huutafuta ufunguo huo.

⁴⁵ Kama vile hapa muda fulani uliopita walipata atomi, na wakajua kulikuwako na atomi, na kisha atomi zikafanya molekuli na kadhalika. Sasa, wakaendelea kuchunguza, mtu fulani aliamini ya kwamba kama atomi hiyo ilishikilia kila kitu pamoja, kama atomi hiyo ingeweza kubadilishwa, hiyo ingechukua kile inachoshikilia na kukivunja vipande. Sababu, kila kitu kimeshikanishwa pamoja kwa atomi, tunajua jambo hilo. Sasa, nguzo ile imeshikanishwa kwa atomi. Wewe umeshikanishwa kwa atomi. Nyasi, miti, kila kitu kimeshikanishwa kwa atomi. Vema, kama hiyo atomi, ikigeuka kabisa, kama inaweza kuvunjwa na kurudishwa, basi ingeamaliza. Na, sasa, wanasayansi wakuu wanaamini ya kwamba hilo lingeweza kufanywa, nao walifanya kazi zaidi na zaidi, na wakaketi saa baada ya saa, na juma baada ya juma, mwaka baada ya mwaka, mpaka hatimaye wakaishinda.

⁴⁶ Ilikuwa, ninaamini, Thomas Edison, juu ya nuru, ambaye wanasema mtu huyo alikuwa na maarifa ya kwamba angeweza kufanya nuru ya umeme. Yeye ndiye mvumbuzi wa glopu ya umeme. Wala hata asingeenda kulala usiku. Angechukua sambusa mkononi mwake na kula chakula chake, na kuketi pale na kufikiria na kufanya kazi. Mahali fulani huko nyuma ya akili yake kabisa, kitu fulani kilimwambia angeweza kufanya jambo hilo. Ni kitu gani? Ni ufunguo unaoweza kuifungua njia.

⁴⁷ Si miaka mingi iliyopita, kulikuwako na m—mtu ambaye aliamini ya kwamba alikuwa na kipaji cha kuandika vichekesho. Aliamini aliushika ufunguo huo mkononi mwake. Naye alitaka . . . alienda . . . Aliishi huko Kansas. Alimwendea mhariri wa gazeti kuu katika Jiji la Kansas, naye akapeleka baadhi ya maandishi yake. Ndipo huyo mhariri akasema, “Bwana, kweli wewe hunacho. Wewe, hakuna haja ya kujaribu, wewe, wewe huwezi kufanikiwa.” Bali hilo halikumridhisha. Alijua alikuwa nacho. Basi akarudi tena na tena, akijaribu, bali huyo (mhariri) angemkatalia. Hatimaye, akaenda mahali pengine, nao wakamkatalia, wakisema, “Bwana, kwa kweli hunacho kabisa. Huwezi kufanikiwa.” Lakini hata hivyo aliamini ya kwamba angeweza kufanya jambo hilo. Na hivyo ndivyo, yeye ana kitu fulani mkononi mwake! Hatimaye, alipata kazi ya kuandika maandishi madogo ya, ninaamini, uhariri ama kitu fulani kwa kanisa fulani, namna fulani ya ucheshi mdogo kwa ajili ya kanisa. Ndipo akajikodishia gereji iliyojaa panya, ambapo panya walikuwa wakikimbia kila mahali humo na kadhalika, katika mashuka yake, ndipo akaona tabia za mtoto fulani wa panya. Hapo ndipo hadithi ya Panya Mkejeli ilipozaliwa. Sasa ni Walt Disney ya milioni nyingi sana. Kwa nini? Yeye alikuwa na kitu fulani mkononi mwake, naye alijua alikishika,

alijua angeweza kufanya jambo hilo. Na hivyo ndivyo kila ufanisi mkuu unavyofanywa. Wakati wanaume na wanawake wanapokuwa na kitu fulani mkononi mwao, kwamba wanajua wanaweza kufanikiwa.

⁴⁸ Wakati polio ilipolivamia taifa hili. Kama vile, sote tumeamriwa sasa kwenda kupata chanjo hii, kuiangamiza. Wakati polio ilipovamia... Jana nilikuwa nikimsikiliza daktari mmoja nilipokuwa nikiendesha gari barabarani, daktari fulani kutoka Louisville. Yeye alisema, “Miaka michache iliyopita, wakati yale maafa makuu yalipoukumba Louisville,” akasema, “laiti watu wangelisimama mahali niliposimama, na kuona vipumulio hamsini na saba kwa wakati mmoja, na wanaume, wanawake, wavulana kwa wasichana, wamepoozwa na ugonjwa ulioitwa ‘polio,’ wala hakuna jambo lingaliweza kufanyika juu yake.” Kasema, “Nisingetaka kuona jambo kama hilo tena.”

⁴⁹ Lakini sayansi iliwazia, “Kama kuna uovu kama polio, hakika kuna kitu fulani cha kuukabili.” Walipambana, walisimama mitaani wamevaa mabuti, hao zimamoto, walitoa kofia, na kuomba misaada, wakaombaomba, wakafanya kila kitu, wakijaribu kupata ufunguo wa kuufungua mlango wa kuwekwa huru. Ndipo, hatimaye, muungwana mmoja Mkristo jina lake Salk akapata hiyo chanjo. Kwa nini? Uovu ulikuwa umejitokeza, mwuaji alikuwa amejitokeza; kulikuwako na ufunguo mahali fulani ambao ungemfungulia mwanadamu uhuru tena, nayo chanjo ya Salk ilikuwa ndiyo tiba kuu. Loo, jinsi ufunguo unavyoweza kufanya! Hiyo chanjo ililetwa, na sasa inaondolea mbali polio kwa chanjo hii, kwa sababu ilikuwa ni “kutochoka na kutokata tamaa,” ufunguo huo ulikuwa mahali fulani. Kulikuwako na kitu kingemchanja mtu, nao waliyakinia kukipata.

⁵⁰ Na kama kuna uovu kama polio, dondakoo, ndui, homa ya manjano, pepopunda, ukakamavu wa viungo, na kadhalika, ambayo sayansi... maovu haya, imeweza kuyapiga vita, usiku na mchana, mpaka wakapata chanjo kutoka kwake, kwa sababu ni ovu, ni uuaji, ni zaidi jinsi gani kwamba pana ufunguo wa wokovu kwa ajili ya mwanadamu ambaye yuko katika gereza la dhambi? Kuna ufunguo wa mlango huo, kuwaweka huru wanadamu kutokana nayo.

⁵¹ Ufunguo, kwa kawaida, wakati unapofungua kufuli, na, unapoupata ufunguo, hauna budi kuwa ni wa hazina fulani, kitu fulani ambacho ni cha thamani, vinginevyo wewe usingekifungia. Kama hakifai kufungiwa, kiache tu. Bali kikiwa kinafaa kufungiwa! Kwa hiyo ufunguo kwa kawaida ni—ni mwelekeo kwa kitu fulani, ama ni njia ya kuingia kwenye kitu fulani cha thamani. Ufunguo, hiyo ndiyo kazi yake, sasa, utafungua kitu fulani kilicho cha thamani.

⁵² Sasa tunasoma katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 10, Yesu alisema, “Mimi Ndimi Mlango wa zizi la kondoo. Mimi Ndimi Mlango,” sio mlango *fulani* “ule Mlango, Mlango wa pekee. Mimi Ndimi Njia, Njia pekee, Kweli, na Uzima, wala hakuna mtu ajaye kwa Baba ila kwa njia ya Mimi. Mimi Ndimi Mlango wa zizi la kondoo na wote wanaonitangulia Mimi ni maadui, wezi na wanyang’anyi.” Yeye Ndiye Mlango wa zizi la kondoo. Yeye Ndiye Mlango wa wokovu.

⁵³ “Hakuna jina lingine lililotolewa chini ya Mbingu liwapasalo kuokolewa Kwalo, ni kupitia tu kwa Jina la Yesu Kristo.” Hakuna kanisa, hakuna dhehebu, hakuna kanuni za imani, hakuna fundisho la chochote; ni kwa Jina la Yesu tu. Huo ndio—huo ndio ule Ufunguo. Si ajabu Petro angeweza kutumia mmoja wa hizo kwenye Siku ya Pentekoste! Wao walitaka kujua jinsi ya kuingia kwenye Mlango huo. Akatumia ule Ufunguo. Na kuna Ufunguo mmoja tu, kwa maana kuna Mlango mmoja pekee. “Mimi Ndimi Mlango.” Naye Petro alikuwa na Ufunguo Wake. Naye akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi yenu, nanyi mtapokea hazina za Mungu.” Ndio Ufunguo wa Mlango, na Yesu Ndiye Mlango.

Kuna Mlango mmoja tu kwa uponyaji, naye Yesu Ndiye Mlango huo.

⁵⁴ Kuna mlango mmoja tu kwa Amani. Naam. “Amani Yangu nawapa ninyi.” Yeye Ndiye ule Mlango mmoja tu kwa amani ya kweli. Huenda ukafikiria una amani. Huenda ukakusanya fedha za kutosha kujinunulia nyumba, huenda ukakusanya fedha za kutosha kuwanunulia watoto wako nguo, mwe na chakula cha kutumia, bali huenda umekusanya umaarufu vya kutosha kupendwa na watu. Lakini wakati unapovua viatu vyako usiku na kujiandaa kulala, kuna Jambo Moja tu linaloweza kukupa amani. Hilo ni, kama ulijua ulikuwa utakufa usiku huo, kuna Amani moja tu, na, hiyo ni kusema, Yesu Ndiye Amani hiyo. Yeye Ndiye Amani yetu.

⁵⁵ Yeye Ndiye uponyaji wetu. “Mimi Ndimi Bwana Mungu wako niyaponyaye magonjwa yako yote.”

⁵⁶ Yeye Ndiye Mlango wa Mbinguni. Wala hakuna mlango mwingine wala hakuna njia nyingine bali ni kwa njia ya Yesu Kristo. Yeye Ndiye Mlango wa Mbinguni.

⁵⁷ Na sasa Yesu Ndiye Mlango kwa mambo haya yote, nayo imani ndiyo ufunguo unaoufungua Mlango huo. Sasa, kama Yesu Ndiye Mlango wa ahadi hizi zote za Mungu, imani katika kazi Yake iliyomalizika hufungua kila mlango wa kila hazina iliyomo ndani ya Ufalme wa Mungu. Mnaliona? Ufunguo ni... Imani ndiyo ufunguo unaoufungua kila ahadi anayoifanya. Ufunguo wa imani hufanya hivyo, imani katika kazi Yake iliyomalizika. Funguo hizi ndizo tunazonena habari zake.

⁵⁸ Sasa katika Waebrania, mlango wa 11, nina mlolongo mkubwa wa hao ulioandikwa hapa chini, wa mashujaa hawa wa imani. Ilikuwa ni ufunguo wa—wa Mlango, ndio uliovivungua vinywa vya simba. Ilikuwa ni ufunguo, imani, ndio uliozifungua nyumba za jela. Ilikuwa ni imani, ufunguo wa imani, ndio uliozima nguvu za moto, ukawaokoa na makali ya upanga, ukawafufua wafu tena. Ilikuwa ni imani, ufunguo wa imani katika Mungu aliye hai. Mkono huo, mwanamume huyo, mwanamke huyo, ambaye anaweza kuuchukua ufunguo huo wa imani, wanaweza kufungua kila ahadi aliyofanya Mungu. Bali kama huna ufunguo huo, unatangatanga tu, kamwe hutaweza kuufungua. Utaupigapiga tu, kwa sababu ufunguo huu. . .

⁵⁹ Ufunguo wowote ulioundwa vizuri una nyenzo ndani ya kufuli, na unachukua umbo fulani, muundo fulani wa funguo hizo kuzungusha nyenzo hizo. Na nyenzo moja tu ndogo ikiondoka mahali pake, itakivuruga kitu hicho chote.

⁶⁰ Kwa hiyo, ninaamini katika Injili yote, kila Neno la Mungu, linalofungulia nguvu za Mungu, linalowafungulia watu baraka Zake. Ni ufunguo wa Mlango, unaoufungua. Loo, hao mashujaa mashuhuri, hao manabii na watu mashuhuri wa Biblia, waliokuwa na ufunguo huo! Hiyo ndiyo sababu waliweza kufunga kinywa cha simba, kuzima nguvu za moto, kuepuka makali ya upanga, kuwafufua wafu tena, na kufanya kila namna ya miujiza, ni kwa maana waliushikilia ufunguo huo nao walijua ulifanya kazi, kwa kuwa ulikuwa ufunguo uliozaliwa na Maandiko.

⁶¹ Sasa, kama ninatangatanga kwa ufunguo wa kanuni za imani, sijui utafanya nini. Kama wao wakisema, “kanisa langu hunena kama *huu*,” sijui hayo.

⁶² Bali wakati Biblia inapolifundisha, nami ninaushikilia ufunguo wa imani mkononi mwangu, ama moyoni mwangu, ambao unasema “hilo ni Neno la Mungu,” huo utazima nguvu za moto, utafungua uponyaji kwa ajili ya wagonjwa, utafungua wokovu kwa waliopotea. Sina budi kuja kwenye Mlango huo, kila kitu kiko katika Jina Lake. “Kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina Lake.” Ukijua ya kwamba ufunguo ulio nao ni imani, kwa sababu ni ufunguo uliotengenezwa kwa Maandiko. Sasa, kama ni ufunguo wa kanuni za imani, ufunguo wa kimadhehebu, sijui utakalofanya. Bali kama ni ufunguo wa Kimaandiko, utafungua, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Sasa, loo, si ajabu waliweza kuzima nguvu za moto, na kadhalika, walikuwa na ufunguo.

⁶³ Ashirio la kwanza la Mungu kwa mmoja wa hao manabii, hakuna kitu kingaliweza kuwazuia. Haikumbidi kufanya kama anavyonifanyia mimi wakati mwingine, kulishindilia tena na tena, na labda kwako wewe (natumaini sivyo), bali anaendelea kuniambia, “Nenda kafanye hivi,” halafu utasitaita

njiani, “Basi nenda kafanye *hivi*,” na “Rudi ukalifanye tena, hukulifanya ipaswavyo.” Ashirio moja tu dogo! Ninii tu, waliweza tu kusikia Roho akiwaambia, “Ndilo jambo la kufanya,” wala hakuna kitu kitakachowazuia. Ndugu, wao—wao—walivifunga vinywa vya simba, waliokoka na makali ya upanga, walizima moto, walifanya kila kitu. Ashirio moja tu kutoka kwa Mungu, kwa sababu waliushika ufunguo huo mkononi mwao, ile imani kuu! Walimfanyia Mungu mambo kwa maana hakuna kitu kitakachowazuia. Loo, ni la utukufu jinsi gani!

⁶⁴ Kama vile kijana mmoja wakati mmoja alivyomjia ndugu mzee ambaye alikuwa ni mzee mcha Mungu, nabii mzee wa Mungu. Naye alimsikia mtu huyo akishuhudia sikuzote, akisimulia wema wa Mungu sikuzote, na jinsi Mungu alivyokuwa, na kile Kristo alichokuwa, na kuendelea tu, akizungumza. Hatimaye, kijana mwanamume huyu alikuwa akienda kufanywa mhudumu hudumani, kwa hiyo akamjia maskini mzee huyu mwenye hekima, naye akamwambia, “Bwana, ninataka kukuuliza swali.”

Akasema, “Uliza, kijana.”

⁶⁵ Akasema, “Kweli Kristo anamaanisha kwako kadiri unavyosema anamaanisha?”

⁶⁶ Akasema, “Yeye anamaanisha mengi sana kwangu kuliko ninavyoweza kuwa na pumzi ya kunena!” Haya basi. Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alikuwa ameupata ufunguo.

⁶⁷ Kijana mwanamume huyo akasema, juu ya hayo, “Kama unayadai mambo haya, nawe unaniambia ya kwamba ni halisi kama ulivyo wewe, basi ninataka kumjua Yesu yuyo huyo, katika uhalisi uo huo.” Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alijua mzee huyo alikuwa ameushika ufunguo, kwamba angeweza kufungua na kufunga.

⁶⁸ Unajua, ufunguo unaofunga, hufungua, pia. Unaona? Unaweza kufungulia ama kufunga. Hiyo ni kweli. Ufunguo ule ule unaofunga, hufungua. Ufunguo unaofunga, unaweza ukafunga. Na hiyo ni kweli kabisa, unaona, kwa sababu unafanya kazi kwa njia zote mbili. Ni huzuni jinsi gani kwamba kanisa lilipoteza kabisa ono lake kwa jambo hilo! Lilikuwa ni jambo la kuhuzunisha jinsi gani wakati kanisa lilipojiuza kwa kanuni za imani, kama tulivyofanya siku hizi, na sasa tunaitwa kuungana.

⁶⁹ Tumeona ambapo ule ukasisi mkuu wa Kirumi na hao wengine wataenda kukutana sasa, watabadilisha sehemu ya ratiba. Nilifikiri hawakubadilika; bali watabadilika, kwa vyovyote, wampe kila kasisi nguvu za papa, na—na popote alipo, na kadhalika. Ni huzuni jinsi gani, kwamba kanisa lilijiua kabisa kwa mafundisho ya sharti badala ya Neno. Unaona? Hapo ndipo wameuacha ufunguo, papo hapo. Hiyo ndiyo sababu ile

miujiza mikubwa na ishara hazifanyiki miongoni mwa watu siku hizi, zilizokuwako, wameupoteza ule ufunguo! Naam, wanaujua Mlango, wanajua Mlango upo, ila jambo linalofuata ni ule ufunguo wa kuufungua Mlango. Hazina ziko nyuma ya Mlango. Zimefungiwa ndani, zisiweze koonekana, na wasioamini. Lakini mwaminio, aliye na imani na anaweza kuuchukua ufunguo wa imani, anaweza kuifungua Milango hii. Naam, bwana.

⁷⁰ Wakati mmoja hapa miaka michache iliyopita, kulikuwako na ndugu mmishenari, naye alijisikia alikuwa na wito wa kwenda Afrika. Alikuwa ni mwanamume kijana; mke na watoto wawili, wazuri sana, hao wasichana wadogo, umri wa miaka saba ama minane hivi, kila mmoja. Basi maskini jamaa huyu mdogo asingeweza kuuondoa kwake. Alikuwa ni m—mhudumu, alikuwa na kanisa zuri nchini. Bali kamwe asingeweza kuondokana na wito huo, yeye “hana budi kwenda huko Afrika.” Naye akaomba, usiku na mchana. Hakutaka kwenda. Na Mungu akashikilia kusema naye, “Lazima uende!” Basi hatimaye akafikia mahali mpaka yeye, shindano la kuamua, ambapo, yeye—yeye hana budi kwenda!

⁷¹ Kwa hiyo akaenda kwenye halmashauri ya umishenari ya kanisa lake, naye akasema, “Mungu ameniita kwenye huduma ya kimishenari huko mbali sana misituni mwa—mwa Rhodesia.” Na katika msitu huu kumejaa malaria, na homa na hilo jua kali, tauni na ukoma, na kila namna ya magonjwa huku ndani ndani katika msitu huu, ndiko alikokuwa anaenda kufanya, kutumia maisha yake yote. Akauza nyumba yake na yote aliyokuwa nayo. Kwa hiyo halmashauri hiyo ya kimishenari ilitaka kumjaribu, nao wakasema, “Hivi una hakika sasa?”

Yeye akasema, “Nina hakika kabisa.”

⁷² Wakamwambia, “Bwana, umewazia jambo hili, ya kwamba una wasichana wawili wazuri sana, na una mke kijana a—anayependeza, na kama unaninii tu . . . Kwa nini usiende tu kule uone jinsi kulivyo kisha urudi?”

⁷³ Akasema, “La, Bwana aliniambia. Loo, ni halisi sana!” Akasema, “Bwana aliniita. Na mimi—mimi sitaki kuondoka nyumbani kwangu, sitaki kuliacha kanisa langu na watu wangu, bali Bwana aliniita kule ndani kwenye msitu huo.”

⁷⁴ Naye akasema, “Bwana, hivi ulijua ya kwamba wasichana wako wadogo wangeweza kushikwa na homa ya manjano ama homa ya maji meusi, na kufa, kwa ghafla sana?” Naye akarejea kwa watu mbalimbali waliokuwa wamewapoteza watoto wao, hao jamaa wadogo, kuwapeleka mle ndani, kwenye magonjwa ambayo hawakuwa na chanjo yayo. Ndipo akasema, “Wazia juu ya ukoma, juu ya mke wako mrembo na wasichana wako wadogo wakiwa na ukoma, na hilo jua kali na kadhalika ambalo unapaswa kuvumilia.” Kasema, “Hivi huogopi, na hiyo hatari ya kuwapeleka watoto wako na mkeo mahali kama hapo?”

⁷⁵ Ndipo mmishenari huyo akasimama hapo, mtu huyo kijana, nayo machozi yakaanza kutiririka mashavuni mwake, akageuka, akasema, “Ndugu zangu! Ono langu la wito wa Mungu,” akasema, “kama Mungu ameniita niende Afrika, watoto wangu na familia yangu wako salama zaidi huko Afrika kuliko mahali pengine popote ulimwenguni.” Amina. Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alikuwa na ufunguo wa wito wake, alikuwa na imani katika yale aliyokuwa akinena habari zake. Loo, nikawazia, ni tamshi la kishujaa jinsi gani! Wakati niliposikia jambo hilo kwa mara ya kwanza, moyo wangu ulidundadunda. Unaona, “Kama Mungu ameniita kwenda Afrika, watoto wangu katika ukoma na tauni na chochote kile, wako salama zaidi huko kuliko mahali pengine popote juu ya uso wa dunia.” Yeye alikuwa na ufunguo. Huo ndio unaohitajika.

⁷⁶ Unapokuwa na ufunguo, hakuna hofu, hakuna shaka, hakuna swali. Haikubidi kumwuliza mtu mwingine yeyote kuhusu jambo hilo, unajua kabisa. Unao mikononi mwako, unajua la kufanya. Amina. Unajua hesabu yake, unajua mlango utafunguka. Umezihakikisha hizo nyenzo na unajua ni jambo la kweli kabisa, mlango utafunguka wazi kabisa utakapouingiza ufunguo ndani.

⁷⁷ Loo, laiti kanisa lingalikuwa tu na funguo hizo! Laiti kanisa lingalikuwa tu na ufunguo wa imani, tungeweza kufungua mlango wowote, maradhi yoyote, tauni yoyote, ugonjwa wowote uliopo. Ungefunguliwa kwetu kama tu tungalikuwa na ufunguo huu. Mtu huyu alikuwa na ufunguo wa wito wake.

⁷⁸ Kama mtaruhusu ushuhuda wa kibinafsi. Ninakumbuka kama miaka kumi na mitano, kumi na saba iliyopita sasa, karibu, wakati Bwana aliponiambia huko chini mtoni, wakati aliposhuka katika hiyo Nguzo ya Moto ambayo mnaiona picha Yake, Naye akanena nami na kusema, “Utaupeleka Ujumbe huu kote ulimwenguni.”

Nami ninakumbuka kule kwenye Kinu cha Green wakati Yeye aliponena nami.

⁷⁹ Basi nilienda na kumwambia mchungaji, naye akaniambia, kasema, “Billy, ulikula nini usiku huo? Ulishikwa na jinamizi.” Akasema, “Rudi kazini mwako. Unafanya kazi kwenye Kampuni ya Utumishi wa Umma, una kazi nzuri, rudi ukaishughulikia kazi ya—yako, mwanangu.” Kasema, “Ulishikwa na jinamizi. Ulikula kitu fulani.” Hilo halikunisogeza hata kidogo!

⁸⁰ Nilipoanza kwenda kwenye ibada za uponyaji, wengi wenu hapa mnakumbuka Ujumbe wangu asubuhi hiyo, *Kama Vile Daudi Alivyoenda Kukabiliana Na Goliathi*, niliohubiri.

⁸¹ Nao wakaniambia, akasema, “Katika siku za sayansi ya kisasa, wakati tukiwa na kila namna ya utafiti wa tiba, wakati tukiwa na madaktari walio bora sana, wakati kanisa limesahau uponyaji wa Kiungu kwa muda mrefu na kadhalika kwa muda

wa miaka mingi, mingi sana iliyopita, utakabilianaje na jitu kubwa mno kama hilo? Utaondokaje mbele za Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, na kadhalika, na hata Wapentekoste, ambao wameusahau muda mrefu sana uliopita, na wakaingia kwenye kanuni zao za imani? Utakabilianaje, pasipo na madhehebu ama chochote kile kukuunga mkono? Utafanya nini, Bill?" Kwa namna moja, nyingine, halikunisogeza hata kidogo, kwa kuwa nilishika ufunguo mkononi mwangu! Nikasema... Wakasema, "Hakuna mtu atakayekuamini. Hutaweza kufanya jambo hilo. Hakuna mtu atakayekuamini."

⁸² Nikasema, "Sijali. Kuna jambo moja la hakika; Mungu aliniita, na sina budi kwenda kwa sababu Mungu aliniita." Niliushika ufunguo. Yeye alikuwa ameniita, alikuwa amenionyesha, alikuwa ameniambia, nami niliiona Uwepo Wake wakati aliponiagiza, nao ufunguo ulikuwako!

⁸³ Mchungaji huyo akasema, "Ukiwa na elimu ya darasa la saba, na ati unaenda kuhubiri na kuomba mbele ya wafalme na watawala!"

Nikasema, "Hiyo ni kulingana na Neno Lake!"

⁸⁴ Mnamo wakati kama huu mwaka uliopita, ama juma moja ama mawili kabla, wakati nilipokuwa nimekuja kwenye kanisa hili hapa na kuwaambia ya kwamba Bwana Mungu alikuwa amenipa ono la kwenda...kufanya safari ya kuwinda, na m—mnyama fulani nitakayempata, ambaye atakuwa na pembe za inchi arobaini na mbili. Na nilipokuwa nikirudi kutoka kumfuatilia mnyama huyu (mahali ambapo angekuwa amelala, mahali ambapo angekuwa), nikiwa njiani nikirudi ningemwua dubu mkubwa mwenye manyoya ya rangi ya fedha na kijivu. Ndipo nikaenda mahali fulani hapa, na nikazungumza na mtu huyo, naye akasema, "Sina habari juu ya mnyama yeyote mwenye sura kama hiyo. Na tukinena juu ya dubu mkubwa mwenye manyoya ya rangi ya fedha na kijivu, kamwe sijapata kumwona mmoja."

Nikasema, "Lakini mahali fulani hana budi kuwa hapa."

⁸⁵ Kwa hiyo akasema, "Hata hatuendi kwenye maeneo ya dubu. Tunaendea kondoo, mbali sana na mpaka wa msitu." Vema, nikaambatana naye.

⁸⁶ Na siku ya pili tukiwa huko nje, kwenye mahali pale pale, mahali pale pale hasa ambapo Bwana alisema, huyo hapo yule mnyama. Kwa hiyo wakati nilipoenda na kumpata mnyama huyo, na wakati tulipokuwa tukimchuna ngozi na pembe na kadhalika, kung'oa, akasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani. Wewe uliniambia, siku tatu zilizopita tulipoondoka ka—kambini, ya kwamba ukiisha kumpiga risasi mnyama fulani huyu, ya kwamba tutakapokuwa njiani tukirudi ungemwua 'dubu mkubwa mwenye manyoya ya rangi ya fedha na kijivu.'"

Nikasema, "Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI!"

⁸⁷ Kasema, “Sitilii shaka,” akasema, “kwa maana ndugu yangu alikuwa na kifafa, wala hukuwahi kumwona maishani mwako, wakati ulipokuwa hapa juu wakati mmoja, nawe ukaniambia mvulana huyo ataponywa nikiisha kufanya jambo fulani. Naye aliponywa.” Akasema, “Sasa, lakini, Ndugu Branham, ninataka kukuuliza,” akasema, “ninaweza kuona huko kote mpaka kwenye mlima ule hata mahali mpaka wa msitu ule ulipo, mahali wale farasi wamesimama. Wala hakuna kitu pale. Hamna hata chembe ya unyasi, hakuna mwamba, hakuna chochote.” Kuvumwani wa kuro, ambao una urefu wa karibu inchi mbili, juu ya mipaka ya misitu, yapata maili moja ama mbili juu ya mpaka wa msitu. Kasema, “Je! dubu huyo atakuwa wapi?”

⁸⁸ Nikasema, “Mungu ni Yehova-Yire. Kama ameniambia kutakuwako na dubu pale, kutakuwako na mmoja pale.

⁸⁹ Wakati tukishuka mlimani, karibu kila wakati tulipofikia nusu maili ama kitu kama hicho, kukaribia zaidi, yeye alisema, “Ndugu Branham, ni karibu na wakati ambapo huyo dubu anapaswa kujitokeza.”

Nikasema, “Usijali, atatokea.”

⁹⁰ Ndipo tulipokuwa ndani ya yadi mia tano karibu na mahali walipokuwa wale farasi, ilitubidi tupumzike tena na zile pembe nzito na kadhalika mgongoni mwetu. Ndipo akaangalia kotekote tena, nami nikauona uso wake wakati aliponiangalia, kana kwamba ndani ya moyo wake alikuwa akishangaa. Unaona, yeye alikuwa *ametumainia* angekuwako, bali hakuwa na ule ufunguo.

⁹¹ Lakini kwa namna fulani, kwa neema ya Mungu, kamwe Yeye hajaniacha. Wakati aliponiambia kungekuwako mwenye manyoya yenye rangi ya fedha pale, mimi nilikuwa na ule ufunguo. Sikulitilia shaka hata kidogo, hata kidogo. Nilimgeukia, na nikasema, “Bud, atakuwako.” Na wakati tu nilipogeuka, huyo hapo yule dubu [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] amesimama papo hapo juu yetu, karibu nusu maili.

⁹² Akavaa miwani upesi, akasema, “Billy, naomba heri, ni mkubwa mwenye manyoya yenye rangi ya fedha!”

⁹³ Unaona, ule ufunguo, ono, Neno la Bwana, hakuna kitu kinachoweza kulibadilisha wala kulizuia. Kile kanisa linachohitaji usiku wa leo si elimu. Kile kanisa linachohitaji usiku wa leo si dhehebu. Kile kanisa linachohitaji usiku wa leo si kanuni ya imani. Kile kanisa linachohitaji usiku wa leo ni ufunguo wa Maandiko, ule Mlango. Ambao, Kristo Ndiye Mlango, Naye ni Neno. Imani katika Neno la Mungu aliye hai huufungua kila mlango.

Mungu, tupe ufunguo. Tupe ufunguo.

⁹⁴ Waebrania, mlango wa 12, inasema, “Basi sisi kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na kutokuamini kule

kutuzingako kwa upesi.” Inasema “dhambi,” ambayo, *dhambi* ni “kutokuamini.” Unaona? Kuna dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini.

⁹⁵ Na *dhambi* inamaanisha “kukosa shabaha.” Kama wakati unapiga risasi, unakosa shabaha, ni afadhali uirekebishe bunduki yako, unaona, kwa maana kuna kasoro fulani. Ulikosa shabaha. Unaona, rudi na ujaribu tena. Unaona? Inamaanisha kugeuka, umekosa shabaha. Unapotaka kuwa Mkristo, nawe unaenda na kujiunga na kanisa, umekosa shabaha. Unapotaka kuwa Mkristo, nawe umenyunyiziwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” umekosa shabaha. Afadhali urudi. Hatalenga shabaha. Utatapanya, hakika kabisa. Kuna Kitu kimoja tu kinachoweza kukushikilia kwenye mstari mkamilifu, hicho ni Maandiko, Biblia, Neno. Kwa kuwa, zote mbingu na nchi zitapita, bali Neno la Mungu halitapita kamwe.

⁹⁶ Kwa hiyo, ushikilie ufunguo, imani katika Neno! Na kila chembe ya imani unayoamini, wala usishuku hata chembe moja, unaweza kuufungua kila mlango unaosimama kati yako na baraka alizo nazo Mungu kwa ajili yako. Mungu na atusaidie kuwa na hizo funguo, ndilo ombi langu. Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi.

⁹⁷ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru usiku wa leo ya kwamba Wewe umetupa ufunguo wa kutufungulia wokovu. Ni—ninakushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Bwana, kwamba tumeokoka, na kwa ajili ya ufunguo ambao tumeweza kuutumia umbali huu. Lakini, Mungu, tupe imani, ili kwamba kila moja ya Maneno haya yaliyoandikwa katika Kitabu Chako ni nyenzo ndogo, nao Ufunguo huu unaoitwa Yesu. . . Mlango huu, ninamaanisha, unaoitwa Yesu; na ule ufunguo, unaoitwa imani, unapogusa kila Neno, hulifungua. Husukuma ule wenzu mdogo chini nasi tunaweza kuingia kwenye hiyo baraka. Baba wa Mbinguni, tupe funguo hizo, tupate kuwa na imani katika ahadi za Mungu, kusudi imani yetu isishindwe, tupate kukutumikia Wewe na wale tunaoshirikiana nao.

⁹⁸ Samehe kila dhambi ya kutokuamini kwetu, Bwana, na utusaidie kuwa Wako. Tunakuja sasa kwenye meza ya ushirika, nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utatusamehe makosa yetu yote, tupate kuingia katika furaha ya ushirika kwenye meza ya Mungu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁹⁹ Ndugu yangu, dada, kama una ufunguo wa Ufalme, ufunguo wa Mlango, ufunguo wa wokovu, Mungu na akusaidie kuifungua milango na hebu Yesu aingie ndani. Naomba akupe mambo unayo—unayotamani sana.

¹⁰⁰ Sasa, hebu kidogo tu kabla hatujaanza kusoma juu ya ushirika, ninataka kusema jambo fulani kwa sababu ni juu ya ushirika. Basi tunapokuja kwenye madhabahu hii, kuna njia moja pekee ya kuja, hiyo ni, kama tumeushika ufunguo wa

imani mikononi mwetu, ambao unatufanya tujue ya kwamba dhambi zetu zimesamehewa. Na kama hatuna ufunguo huo wa kuufungua Mlango huo, kwamba dhambi zetu zimesamehewa, hatuna shughuli kwenye meza ya Bwana. Kwa sababu, kila alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana. Sasa, hiyo ni kweli.

¹⁰¹ Nadhani sisi sote tunajua ya kwamba leo ni Siku ya Ushirika Nchini. Hii ndiyo siku ambayo makanisa yote wanakula ushirika. Ndiyo Siku ya Ushirika Nchini kote nchini. Nami nilidhani ya kwamba lingekuwa ni jambo jema kusema neno moja ama mawili juu ya ushirika kabla hatujaula, wakati mchungaji, akipenda, anapoyaandaa Maandiko ya kusoma ya u—utaratibu wa meza ya Bwana. Sasa, ushirika huu... Sasa, sitachukua ila kama dakika kumi.

¹⁰² Ushirika huu tunaajiandaa kula, umekuwa ndio ubishi mkuu sana wa fundisho lolote katika Biblia. Huo ulikuwa ndio ninii wao... mmoja wa ubishi wao wa kwanza katika lile kanisa la mwanzoni. Na siku hizi Protestanti, wa Episkopolia na Wamethodisti, na mengi ya makanisa ya Kiprotestanti, wangeikubali Katoliki kwa furaha, fundisho la Katoliki ya Kirumi, kama wangepata kuutatua huo ubishi mdogo wa ushirika. Lakini watakubali kwamba kasisi anapaswa kuoa na kuwa wahudumu, kanisa Katoliki lilikubaliana na jambo hilo mara nyingi katika mikusanyiko na mikutano yao. Wanakubaliana juu ya hilo. Nao watakubaliana juu ya maombi mbalimbali, na kadhalika, kanisa la Kiprotestanti litakubaliana na jambo hilo. Na katekismo na kadhalika, madhabahu ndogo hapa na pale, na kanisa Katoliki liko radhi kufanya hivyo. Bali inapofikia ushirika, hapo walianguka. Mtu yeyote aliyepata kuisoma historia anajua hilo. Lakini, hakika, nionavyo mimi, wangepata na mengi ya kuacha, kabla si—sijalikubali, mnaona, kwa maana si Biblia.

¹⁰³ Bali nawatakeni mliambie kanisa Katoliki jambo moja. Je! mnajua ya kwamba kanisa Katoliki, hapo mwanzoni, lilikuwa kanisa la kipentekoste la kimitume? Hakika lilikuwa! Lilikuwa ndilo kanisa la kwanza. Nanyi mnaona mahali wao—mahali wamefikia, waliendelea kuliondoa Neno na kuingiza fundisho la sharti.

¹⁰⁴ Na kama kanisa la Kipentekoste likidumu miaka mingine mia moja, litakuwa mbali sana na Biblia kuliko kanisa Katoliki lilivyo siku hizi, kulingana na jinsi linavyoendelea sasa.

¹⁰⁵ Ililichukua kanisa Katoliki, miaka mia kadhaa kuliacha, miaka mia tatu, kutoka kwenye kanisa la mwanzoni mpaka kwenye kuliundia dhehebu kanisa Katoliki la Kirumi, ambalo walilianzisha. Nao wameshika, wakiingiza waungwana mashuhuri na kadhalika, wakaondosha *hili* na kuingiza *hili*, na kuondoa *hili* na kuingiza *lile*, na kushusha sanamu za kipagani

na kuinua sanamu za Kikristo, na kadhalika, na kupatana tu kwenye Hilo mpaka wakafikia kile walicho nacho sasa, Kanisa Katoliki la Kirumi.

¹⁰⁶ Nalo kanisa Protestanti la Kipentekoste kutoka kwenye ile—ile miaka hamsini limedumu, na mahali lilipoanguka kutoka mahali lilipoanzia, litakuwa kwenye hali mbaya kuliko kanisa Katoliki, miaka mia moja tangu sasa. Hiyo ni kweli. Hilo ni neno kubwa la kusema, bali angalia tu mahali walipotoka wakaanguka. Waliingia moja kwa moja katika dhehebu, waliingia moja kwa moja kupatana juu ya *hili* na *lile*, na chochote kile. Nao hao hapo wanaenda, unaona, wanarudi moja kwa moja.

¹⁰⁷ Lakini, *ushirika*, unaitwa “meza ya Bwana.” Sasa, watu wengi, wanataka kuula asubuhi. Haikusemwa katika Biblia ya kwamba ulikuwa ni *kiamshakinywa* Chake. Na jinsi watu hawa siku hizi, jinsi ambavyo wangali wanaweza kusema “chakula cha jioni cha Bwana,” na hawatekelezi hilo. Wameondolea mbali *chakula cha jioni*, na kuacha hilo, na kuuia “chakula cha kutwa,” upuuzi. Chakula cha jioni!

¹⁰⁸ Sasa, imekuwa ni ubishi daima katika nyakati za Biblia, ilikuwa ni ubishi wakati huo. Watu walielewa vibaya meza ya Bwana, walipokuja mezani. Paulo aliwaambia wale Wakorintho. Walikuwa wakija na kulewa kwenye meza ya Bwana. Unaona, ilieleweka vibaya wakati uo huo. Yeye alisema, “Mkitaka kula, kuleni nyumbani.”

¹⁰⁹ Na jambo lingine, ulieleweka vibaya, kwamba ulikuwa ni nini. Wenye dhambi, na mtu anayeishi katika dhambi, alikuja na kula ushirika. Na hilo lilieleweka vibaya. Mtu anayeishi na mama yake, mama wa kambo, na kanisa lilikuwa limemwambia juu ya jambo hilo; bado akila ushirika mezani.

¹¹⁰ Na kulikuwako na faraka kati yao, nao walikuwa bado wanakula ushirika. Akasema, “Nasikia ya kwamba mnaenenda kama hao Wamataifa wengine. Na kuna—kuna faraka miongoni mwenu, kama ilivyo katika—hasa sana katika nyumba ya Kefa, na kadhalika.” Kasema, “Mnaenenda kama hao Wamataifa wengine.” Unaona, ulieleweka vibaya.

¹¹¹ Ushirika daima umeeleweka vibaya. Sasa, ningeendelea na hilo kwa saa kadhaa, bali inatupasa kufanya ushirika huu na kutawadha miguu. Sasa wamekuacha kabisa kutawadha miguu, ila madhehebu machache tu. Wapentekoste wengi wamekuacha kabisa. Mnaona? Na kungali katika Biblia jinsi tu kulivyoandikwa. Mnaona?

¹¹² Sasa, Roma haiuiti “ushirika.” Wanauita “misa, ni misa takatifu.” Wao hawali ushirika, wanakula misa. Ni misa, na misa hakika inaondoa maana halisi kutoka kwenye ushirika. *Misa* maana yake ni “kutumainia.” Wanakula misa, wakitumainia (kwamba katika kufanya hivi katika misa) kwamba Mungu

atawasamehe dhambi zao, kwa kuula “mwili halisi wa Kristo, ambao kasisi anaubadilisha kuwa Mwili na Damu ya Kristo,” wanaula huo, wakitumaini ya kwamba Mungu atazisamehe dhambi zao kwa kufanya hivyo. Ni misa.

¹¹³ Waprotestanti wanauita “ushirika.” Ushirika maana yake ni “kutoa shukrani.” Kwamba Waprotestanti... Wakatoliki wanakula misa, katika misa wakitumaini ya kwamba Mungu atawasamehe matendo yao maovu. Mprotestanti anaula kwa shukrani kwa ajili ya yale ambayo yamefanywa tayari na ushirika pamoja na Mungu; kushiriki pamoja Naye, kwamba tayari imetendeka. Mkatoliki anatumaini ya kwamba imetendeka; Mprotestanti anasema tayari imetendeka. Mkatoliki anashangaa kama dhambi zake zimesamehewa; Mprotestanti anakiri ya kwamba zimesamehewa, ya kwamba yeye ni huru. Na ushirika ni kushiriki pamoja na Mungu. Na vitu hivi tunavyokula, sio katika *matumaini* ya kwamba dhambi zetu zimesamehewa, bali *zimesamehewa*. Kwa sababu ni... Mmoja ni tumaini; na huyo mwingine ni imani. Mmoja anatumaini yuko sawa; na huyo mwingine anajua yuko sawa. Mnaona? Huyu mwingine, mmoja anatumaini, kwa maana hajui anakosimama; huyo mwingine anajua yuko sawa, kwa maana anajua yale Mungu alisema. Jambo ndilo hilo. Hiyo ndiyo tofauti. Kwa hiyo, wakati wewe ukiwa unatumaini tu, kuwa mwangalifu; bali wakati unapojua, basi endelea. Unaona, basi unafanya ushirika pamoja na Mungu. Mprotestanti ni, yeye anasema amesamehewa na anajua jambo hilo; Mkatoliki ana misa, anatumaini ya kwamba atasamehewa. Ni kama hivi tu: mmoja ni mwombaji, akitumaini ya kwamba kila kitu ni shwari, mnaona; huyo mwingine ni mwombaji akitoa shukrani kwa ajili ya yale ambayo tayari yamefanywa. Wote wawili ni waombaji. Lakini mmoja anaomba, akitumaini atapata kitu hicho; mwombaji huyo mwingine anajua amepata kitu hicho, naye anamshukuru kwa kumpa. Sasa, hiyo hapo tofauti. Huo ndio ushirika. Naam, bwana. Mmoja anatumaini ya kwamba amesamehewa; huyo mwingine anajua amesamehewa, naye anashukuru kwa ajili yake.

¹¹⁴ Kwa hiyo, ushirika ni wa Wakristo waliozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Na *kuzaliwa mara ya pili* sio kwamba inamaanisha kuwa lazima una Roho Mtakatifu. Sasa kumbuka. Sasa, wengi wanafundisha hivyo. “Simjui mtu yeyote anayelifundisha namna hii,” kama mzee Ndugu Arganbright alivyosema usiku ule kutoka hapa mimbarani, mnaona. Lakini, kuzaliwa upya sio ubatizo wa Roho Mtakatifu. Maandiko hayaungi jambo hilo mkono, sidhani, unaona, nionavyo mimi. Unaona? Ninaamini ya kwamba umezaliwa mara ya pili...

¹¹⁵ Na hiyo ndiyo sababu mimi hutumia neno ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, bali sio kwa kuzaliwa upya. Sasa, Pentekoste, Kanisa la United Pentekoste, hubatiza katika Jina la

Yesu Kristo kwa ajili ya wongofu. Siamini hilo. Nao wanaweza kufanya hivyo wakitaka. Lakini ninaamini ya kwamba Petro alisema, "Tubuni," kwanza. Maji hayaiondoi dhambi. Church of Christ linahubiri hivyo. Bali ninaamini ya kwamba toba, hofu ya Kiungu; *tubu* linamaanisha "geuka, rudi ulikotoka," ulikosa shabaha, "anza upya tena." Fanya hivyo kwanza! Na ubatizo wako majini ni onyesho la nje tu la jambo fulani ambalo limefanyika ndani yako, ya kwamba umemkubali Kristo kama Mwokozi wako.

116 Nadhani ni kanisa hili tu hapa usiku wa leo, nijuavyo mimi, mimi sipo hapa vya kutosha kujua ni nani anayekuja ama asiyekuja. Nilipata kukosolewa kidogo hapa si muda mrefu uliopita juu ya kumbatiza mtu hapa kwenye kidimbwi hiki, mzee mmoja. Nami nilimwendea, alikuwa ni mtu mzuri mkongwe. Nilikuwa na majaliwa ya kuiongoza familia yake yote kwa Kristo, wote ni Wakristo. Mzee huyu alikuwa ni mtu mzuri mwenye umri mkubwa, nami nilimpenda, kwa hiyo nilimwendea na kumwambia, "Baba, kwa nini usiwe Mkristo?" Yeye ananipenda.

117 Akasema, "Ndugu Branham, nitakuwa Mkristo wakati ninapoweza kuwa mzuri vya kutosha."

118 Nikasema, "Hebu nikwambie la kufanya, Baba. Wewe angalia kila mahali mpaka utakapopata ambapo unaweza kuwa mzuri vya kutosha, ndipo uniambie mahali hapo ni wapi, ninataka kupaendea, pia." Nikasema, "Kristo kamwe hakuja kumwokoia mtu aliye mwema. Alikuwa kumwokoia aliye mtu mbaya." Unapofikiri kwamba wewe ni mzuri, basi Yeye hakuja kukuokoa. Yeye alikuja kuwaokoa hao anaojua ni wabaya. Unaona? Kristo alikufa kuwaokoa wenye dhambi. Unaona? Kisha nikasema, "Papa, kuna mstari papa hapa."

Akasema, "Vema, ninavuta sigara hizi."

Nikasema, "Mimi hata sitazungumza kuhusu hizo."

Akasema, "Nimejaribu kuziacha, Ndugu Branham."

Nikasema, "Vema, hatutazungumza juu ya sigara."

Akasema, "Vema, nitakapoweza. . ."

119 Nikasema, "Usininii, usiseme zaidi juu ya hizo, zisahau. Ninataka kukuuliza swali."

Akasema, "Vema, ni lipi?"

Nikasema, "Je! unaamini ya kwamba Mungu yupo?"

120 Kasema, "Hakika, ninaamini hilo." Kasema, "Ninaamini hilo kwa dhati kama unavyoliamini, ningedhanja, Ndugu Branham."

121 Nikasema, "Je, unaamini ya kwamba Mungu yuyo huyo alichanganya uzao Wake na akafanyika mwili na kukaa

miongoni mwetu katika utu wa Yesu Kristo, kusudi apate kumwoko mwanadamu?”

Akasema, “Naam, ninaamini hilo.”

“Naye alikufa apate kuwaokoa wenye dhambi kama ulivyo wewe na kama nilivyo mimi?” Unaona?

“Naam, ninaamini jambo hilo.”

¹²² Nikasema, “Sasa, ni hivi tu. Sisi sote tumo kwenye jengo moja kubwa hapa, na tuko gerezani, wala mimi siwezi kusimama hapa pembeni na kusema ‘*hii* itanisaidia kutoka gerezani,’ nisimame pale kwenye kona lile na kusema ‘*ile* itanisaidia kutoka gerezani,’ sote tuko kwenye tatizo lile lile. Na kila mtu aliyezaliwa katika ulimwengu huu alizaliwa katika dhambi, akaumbika katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo. Kwanza kabisa, yeye ni mwasi.”

¹²³ Mtu fulani aliuliza hivi majuzi, akasema, “Ndugu Branham, kama... kungekuwako na tofauti yoyote kati ya Adamu na Hawa, na watoto wao siku hizi, kama wote walikuwa uchi, wakitembea katika... Je!—je! miili yao ingekuwa ni sawa?”

¹²⁴ Nikasema, “La, bwana.” Tulikuwa tukija nyumbani kutoka kuwinda kuchakulo, mimi na Ndugu Fred, na baadhi yao. Nikasema, “La, wasingekuwa wanafanana.”

¹²⁵ Kasema, “Unamaanisha Hawa asingekuwa mwanamke kama binti zake, wala Adamu asingekuwa mwanamume kama wanawe?”

Nikasema, “Kwa njia nyingi, bali si kwa kila hali ya kimwili.”

Akasema, “Tofauti ingekuwa ni nini?”

¹²⁶ Nikasema, “Wasingekuwa na kitovu chochote. Waliumbwa. Kweli. Hawakuwa wameunganishwa na chochote kile.”

¹²⁷ Mradi hicho kinakulia hapo kwenye kila kitu kilichozaliwa katika ulimwengu huu, kwanza kabisa, kinaonyesha ni haini. Hiyo ni kweli. Nikasema, “Hakika, pana tofauti. Wasingekuwa na kitovu. Hawakuwa wameunganishwa na mwanamke yeyote, ili kuja hapa.” Unaona, Mungu aliwaumba.

¹²⁸ Sasa, nikasema, “Ninataka kusema jambo fulani. Kila mtu kwenye jela hili, ni nani aliye mtakatifu? Ni nani ambaye hakuzaliwa kwa kujuana kimwili? Ni nani anayeweza kumsaidia mwenziwe, haidhuru yeye ni nani? Sisi sote tuko kwenye jela lili hili. Lakini Mungu alijifanya Mwenyewe mmoja wa viumbe Vyake na akaja bila kupitia kwa kujuana kimwili, kwa Damu takatifu ambayo Yeye aliumba Mwenyewe, na kupitia Damu hiyo Yeye alitukomboza.” Nikasema, “Je! unaamini hilo, Baba?”

Akasema, “Ninaamini hilo.”

¹²⁹ Nikasema, “Kristo alikufa kwa ajili ya mtu mbaya kama wewe. Sasa, kuna njia moja tu ya kufanya. Hakuna kitu

unachoweza kufanya. Yeye anakupa nafasi hiyo wewe. Huwezi kuistahili. Hakuna unachoweza kufanya kuipata. Yeye anakupa nafasi hiyo bure tu. Je! utakubali yale aliyokufanyia, kukuokoa na kuzimu?"

¹³⁰ Akasema, "Nitafanya hivyo." Akasema, "Lakini laiti ningaliweza tu kuacha sigara hizi."

¹³¹ Nikasema, "Sigara zitajishughulikia. Wewe ninii tu... Sikuombi. Mimi si mshika sheria. Ninaamini katika neema. 'Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu.'" Nikasema, "Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote!"

Akasema, "Kwa moyo wangu wote, ninaamini."

¹³² "Basi utakubali kwenye misingi hiyo, ya kwamba huistahili, bali Yeye Ndiye anayestahili. Usijiangalie; mwangalie Yeye, maana huwezi kujifanyia kitu. Mwangalie Yeye aliyefanya jambo fulani kwa ajili yako. Vipi kumhusu Yeye?"

"Loo," akasema, "Yeye anastahili."

Nikasema, "Haya, basi kubali kile akupacho."

Akasema, "Nakubali."

¹³³ Ndipo nikambatiza katika Jina la Yesu Kristo. Naye akaondoka hapa na kuiwasha sigara.

¹³⁴ Majuma machache yaliyopita nilikuwa huko chini nyumbani kwake. Niliona ono usiku mmoja, la mti usiokauka ukikatwa, ukageuzwa juu chini. Nikaona umepigiliwa ubao. Papo hapo karibu na ubao huo wa mwisho kulikuwako na ubao mzuri wa matangazo. Na chini ya ubao huo, papo hapo karibu na mwisho wake, emeelekezwa *hivi*, mti huo ukavunjika papo hapo. Ndipo Sauti ikasema, "Ilipaswa kuwa wewe," ama, "Ingekuwa ni wewe." Kisha Papa Cox akaanguka, akauponda mgongo wake *hapa* ndani. Na kwa hiyo kesho yake asubuhi wakamletea sigara zake wakati alipokuwa kitandani, ile shauku ilikuwa tayari imemwacha. Majuma kadhaa yaliyopita! Hajapata kuonja hata moja, hata hataki moja ama chochote kile. Mnaona? Nami nilimwona muda mfupi uliopita, wakati mikono yake ilikuwa ni ya hudhurungi kila mahali, majuma machache yaliyopita, kwa sigara, na sasa hata hawezi kuvumilia moja ikiwa karibu naye. Weka mambo ya kwanza kwanza! Usijaribu kuwa mzuri; wewe ni mwovu, kwanza kabisa, wala hakuna kitu unachoweza kufanya. Upo mstari wa kutenganisha, na jamii yote ya kibinadamu iko upande huo.

¹³⁵ Sasa, wakati nilipozaliwa katika ulimwengu huu, ilikuwa ni katikati ya ndoa takatifu, kati ya baba na mama yangu; ndani ya tumbo lake la uzazi kulikuwako na yai, katika tezi za baba yangu kulikuwako na seli ya damu. Uhai wangu ni seli hiyo ya damu (si yai la mama yangu), seli ya damu ya baba yangu. Na wakati hiyo seli ilipoenda mahali pake sahihi kukutana na hilo yai, ilipofanya hivyo, maumbile yaliamriwa na Mungu kunipa mwili.

Ndipo basi hapo nikazaliwa katika jamii ya binadamu, nilipewa nafasi ku—kuwa mtu mwenye akili kama walivyo wanadamu, ambapo ningeweza kuendesha gari, ama ningeweza kufanya mambo kama wanadamu wanavyofanya, kutembea, kuongea, kuendesha motokaa, na kadhalika. Nilipewa hayo, kwa maana nilizaliwa katika familia ya mwanadamu, na kupewa nguvu za akili nipate kuwa mwanadamu.

¹³⁶ Sasa, nilipozaliwa katika familia ya Mungu, nilikuja kwa Damu, Damu ikanipa Uzima. Ndipo baada ya mimi kuwa hai katika Kristo, Yeye alinibatiza kwa Roho Mtakatifu na nguvu, nipate kuwa mwana wa Mungu. Sasa, kama vile tu ningeweza kutembea, kuzungumza kama mwanadamu, kuendesha motokaa yangu kama mwanadamu. Sasa ninapompokea Roho Mtakatifu, ninapokea nguvu za kuwatoa pepo, kusema kwa lugha mpya, kuihubiri Injili, kuwaponya wagonjwa. Nimebatizwa! Sio kuzaliwa; bali kubatizwa!

Walikusanyika kwenye chumba cha juu,
Wote wakiomba katika Jina Lake,
Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Na nguvu za utumishi zikaja.

¹³⁷ Amina. Unaamini hadi upate Uzima wa Milele, na unazaliwa mara ya pili kwa imani yako. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna uzima wa milele,” si Roho Mtakatifu, yuna uzima wa milele tu. Yeye amezaliwa katika familia ya Mungu. Kisha anabatizwa katika Roho Mtakatifu, akiwa na nguvu za akili ya imani, kuiamini Injili na kuitekeleza na kuifanya itende kazi vizuri. Amina. Ndipo anatenda kama mwana wa Mungu. Ndipo anapoweza kutoa pepo. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao!” Mnaona? “Katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watahika nyoka, watakunywa vitu vya kufisha.” Mnaona, yeye anapokea nguvu kwa Roho Mtakatifu, kufanya mambo haya.

¹³⁸ Sasa, wakati alipoondoka, Yeye alisema, “Yafaa Mimi niondoke. Kwa maana, nisipoondoka, huyo Roho Mtakatifu hatakuja.” Mnaona? Ndipo akiisha kuja, ataushutumu ulimwengu kwa habari ya dhambi, na kufundisha haki, na kuwapasha habari za mambo yajayo (hayo ni maono). “Atayachukua mambo ambayo nimewafundisha, na kuwafunulia.” Yale Maneno hasa kwamba Yeye amekuja... Hakuna mtu anayeweza kulifahamu Neno nje ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na wakati mtu anaposema ana ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kukanusha kwamba Neno ni kweli, kuna kasoro fulani.

¹³⁹ Paulo alikuwa ni mkosoaji wa Agano Jipya. Halikuwa, Agano Jipya halikuwa limeandikwa. Paulo alikuwa ni mkosoaji wa Ukristo, Sauli. Na wakati alipompokea Roho Mtakatifu,

alishuka akaenda Asia miaka mitatu na kuyasoma Maandiko, kwa kuwa alifunzwa chini ya Gamalieli, mwalimu mashuhuri. Na ndipo wakati aliporudi, na miaka kumi na minne baadaye, alipanda akaenda kukutana na Petro huko Yerusalemu, na akakuta kwamba walikuwa ni Injili ile ile Neno kwa Neno. Mungu yeye yule aliyemfanya Petro kuhubiri kwenye siku ya Pentekoste na kuwaambia watubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, Roho Mtakatifu yuyo huyo alimfunulia Paulo, naye akawaambia katika Matendo 19 wakiisha kubatizwa wakati mmoja na Yohana, kasema, “Inawapasa kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo.” Mnaona?

¹⁴⁰ Mnaona, Roho Mtakatifu hudumu moja kwa moja na Maandiko. Imani yake katika jambo Hilo hufungua kila siri. Amina. Biblia ilisema, katika Yohana wa Kwanza 5:7, “Wako watatu washuhudia, Mbinguni: Baba, Neno (ambalo lilikuwa ni Kristo), na Roho Mtakatifu. Hawa watatu ni mmoja.” “Kisha wako watatu washuhudia duniani: maji, Damu, Roho. Hawa watatu si mmoja, bali hupatana kwa habari moja.” Sasa, huwezi kuwa na Baba bila ya kuwa na Mwana, huwezi kuwa na Mwana pasipo kuwa na Roho Mtakatifu; hao ni mmoja. Bali unaweza kuhesabiwa haki bila ya kutakaswa, na unaweza kutakaswa bila ya kuwa na Roho Mtakatifu. Utakaso ni kwa Damu, kupitia Damu huja Uhai. Unaona? Naye Roho Mtakatifu ni nguvu za Mungu, unaona, nguvu zilizotolewa kwa kanisa.

¹⁴¹ “Mtapokea” (kitu gani?) “nguvu,” Matendo 1:8, “akiisha kuwajilia juu yenu huyu Roho Mtakatifu. Mtapokea nguvu!” (Si “mtazaliwa mara ya pili.”) “Mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu. Ndipo ninyi ni mashahidi wangu Yerusalemu, Uyahudi, na Samaria, hata miisho ya nchi.” Unaona? Unapokea nguvu ukiisha kumpokea Roho Mtakatifu. Lakini kwanza huna budi kumpokea Roho Mtakatifu, na hizo ni nguvu za Mungu, unaona, kudhihirisha na kuthibitisha. Wewe ni—wewe ni...kama vile ulivyokuwa ni mwanadamu, na ukajifunza kuzungumza na kutembea na kufanya mambo anayofanya mwanadamu; unapobatizwa na Roho Mtakatifu, mnapewa nguvu za kutenda kazi kama wana na binti za Mungu. Si ajabu watu wanatenda na kufanya jinsi wanavyofanya siku hizi, kamwe hawajapata kujazwa na Roho Mtakatifu. Kama wangejazwa, wangeenda tofauti. Wanadai kwamba wamejazwa, bali Yesu alisema, “Kwa matunda yao mtawatambua.” Kwa hiyo unawezaje kufanya jambo hilo, unaona, yote yamevurugika. Unaona? Bali rudi kwenye mambo ya hakika!

¹⁴² Sasa, kama unatembea kwa uaminifu na kudai kwamba wewe ni Mkristo, tunakualika usiku wa leo kwenye meza ya Bwana. Leo, hapana shaka, ushirika umeliwa kote nchini, wengine wao kwa njia moja na wengine katika njia nyingine. Bali nafikiri njia bora zaidi ya kufanya jambo hilo ni kuyafuata

Maandiko, kama vile tu walivyofanya katika Maandiko. Nafikiri hilo lingetosha.

¹⁴³ Je! una Biblia yako, Ndugu Neville? Ndugu Neville sasa atayasoma Maandiko. [Ndugu Neville anasema, “Katika mlango wa 11 wa Wakorintho wa Kwanza, kuanzia kifungu cha 23,” na anasoma Maandiko yafuatayo:

Kwa maana mimi nilipokea kwa Bwana niliyowapa ninyi, Ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate,

Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu uliovunjwa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.

Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.

Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.

Basi kila aulaye mkate huo, na kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.

Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe,

Maana alaye na kukinywa usivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.

Kwa sababu hiyo wako wengi kweni walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala.

Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.

Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.

Ndugu Neville anasema, “Bwana abariki kusomwa kwa Neno Lake.”—Mh.]

¹⁴⁴ Sikuzote ni jambo takatifu sana, jambo tukufu sana, nafikiri inatupasa kuviinamisha vichwa vyetu sasa katika maombi ya kimya. Niombeeni, nitawaombea. Hebu na tuombeane, kwamba Mungu ataturehemu sisi viumbe wasiostahili ambao wako tayari kushiriki sakramenti hii kuu katika ukumbusho wa mauti ya Bwana wetu.

¹⁴⁵ [Ndugu Branham anatulia kwa ajili ya maombi ya kimya. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Maombi haya ya toba tunakutolea Wewe, Baba yetu, juu ya madhabahu Yako ya dhahabu, pamoja na Sadaka yetu, Bwana Yesu. Tunaomba katika Jina Lake. Amina.

¹⁴⁶ Sasa ninaamini wazee watachukua mahali pao, nao wataninii . . . pa kanisa, nao watawaleta watu huku wanapokuja, safu kwa safu, kwa ajili ya ushirika. Daima ninawazia juu ya ule wimbo:

Mpendwa Mwana-Kondoo anayekufa, Damu
Yako ya thamani
Kamwe haitapoteza nguvu Zake,
Hata Kanisa lote la Mungu lililokombolewa
Litakapookolewa, lisitende dhambi tena.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁴⁷ Baba wa neema na Mtakatifu, Yehova, Mwenyezi mkuu, tuma baraka Zako juu ya watu Wako tunapongojea. Zisamehe dhambi zetu. Na sasa tunakutolea Wewe sakramenti hii, divai hii, zabibu ambazo zimekuzwa, nayo mikono ya wahudumu iliziponda-ponda hizi. Nazo zilifanywa divai kwa kusudi ambalo tunaita Kwako sasa, ipate kuwakilisha kwetu Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo. Ninakuomba, Baba, uitakase divai hii kwa kusudi hilo. Samehe kila dhambi yetu. Na jalia kila mtu anayepokea divai hii mwilini mwao, jalia wawe na afya, nguvu, na wokovu kutoka Kwako. Tujalie hilo, Bwana. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁴⁸ Biblia ilisema ya kwamba wakati alipoumega mkate na kuubariki, alisema, "Twaeni, mle, huu ndio Mwili Wangu unaovunjwa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa ukumbusho Wangu." Na wakati tunapokula vipande hivi vidogo vya mkate, vya mkate mwembamba, ambao umeokwa bila chachu. Umeokwa na Wakristo. Umeokwa kwa sababu una—unawakilisha Mwili wa Kristo. Tunaelewa ya kwamba—ya kwamba ilikuwa ni wanafunzi wa siku za Kristo, ama wa siku ya kanisa, ambao walichukua sehemu hizi na kupika chakula cha jioni cha mara ya mwisho, kwenye chakula cha jioni cha mwisho cha Kristo. Na kote katika Biblia, wanafunzi ndio waliowahudumia watu vitu hivi. Na leo hii, wanafunzi wetu wa siku hizi, ndugu zetu hapa wa kanisa, wanafunzi wa Huduma hii, huwahudumia watu. Nao wataavichukua vipande hivi na kuwapa watu.

¹⁴⁹ Na sasa mtakapoupokea mkate huu, kumbukeni, unamwakilisha yule Mwana-Kondoo. Miaka mingi iliyopita wakati mwana-kondoo wa Israeli alipookwa juu ya moto, na akaliwa pamoja na mboga zenye uchungu, watu hao walipata nguvu; viatu vyao kamwe havikuchakaa, nguo zao kamwe hazikupata uchakavu, kote katika safari hiyo mpaka walipofika kwenye nchi yao ya ahadi. Mungu na atudumishe tukiwa na afya, furaha, tukimtumikia mpaka tutakapofika kwenye Nchi ya Ahadi ambayo Yeye ametupa.

Na tuombe.

¹⁵⁰ Baba yetu mwenye rehema wa Mbinguni, ninapozungumza usiku wa leo juu ya ule Mwili Mtakatifu, uliotakaswa wa Bwana wetu, ambaye ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu. Ninapowazia juu ya mwili huo ukipondwa na—na kuvunjwa, na Damu ikitiririka, mgongo Wake na mbavu Zake zikionekana wazi, mijeledi huku na huku mgongoni Mwake; wakati ninapowazia juu ya mkate uliokunyata, uliopigwa unawakilisha jambo hilo, inajitokeza upya mioyoni mwetu. Tunaiweka mioyo yetu, Bwana, juu ya madhabahu Yako usiku wa leo. Tusamehe, Ee Mungu. Na jalia mkate huu uliovunjwa, unapoingia vinywani mwa hawa, watumishi Wako, basi jalia watambue ya kwamba ilikuwa ni Mwili Wako wa thamani uliochubuliwa na kujeruhiwa, na kwa mapigo hayo sisi tumeponywa. Tujalie, Bwana. Utakase mkate huu mwembamba kwa ajili ya matumizi yake yaliyokusudiwa. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Hebu tutulie kidogo tu.

¹⁵¹ Si ushirika wa kundi maalum. Kila mwaminio Mkristo amekaribishwa kwenye meza ya Bwana, kula ushirika huu pamoja nasi.



UFUNGUO WA MLANGO SWA62-1007

(The Key To The Door)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 7 Oktoba, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org